# 158 Liko Pumziko la Mioyo

*Sauti na wimbo: Es ist noch eine Ruh vorhanden* | *Mtunga sauti: K.F. Ellwanger, 1855*

*P.B. I 303, N.K. 120* | *Mtunga maneno: J. S. Kunth, (1700-1779)*




2. Mungu ametuchagulia pumziko lisilo mwisho
Amelitengeneza kale, mtu hajazaliwa bado.
kufa kwamfurahisha Mponya, tupate pa
kupumzikia. Aita, anaalika,
mioyo inayokaa na shida, msikawie, njooni
leo! Ingieni pumzikoni!

3. Ninyi mshindwao na mizigo, mlemewao na
uzito, rukeni kimbieni hima, tokeni pangoni
mwenu; msienende kwa kuinama,
Mponya anawaambieni: "Mimi ni
pumziko lenu, ninyi wana wote wa Mungu.
Popote mwalizwa na shida,
kwa Yesu mwanyamaa kimya!

4. Hapo pumzikeni rahani, wasiwasi hatunao.
Shikeni neno hili jema: "Pumzikeni, Yesu
yuko!" Shikeni mabawa upesi, karukieni kama
ndege; Wako jamaa wanangoja:
Furahi moyo, shangilia, patana nao utukuze,
uko mwaka wa pumziko!